**HOTUBA YA IJUMAA**

**القيم المجتمعية**

**Maadili ya Kijamii**

**Imefasiriwa na**

**profesa Ayman Alasar**

Shukrani njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu. Mwenye kusema ndani ya kitabu chake:

**إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ.**

{**Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa wa karibu; na anakataza uchafu, na uovu, na dhuluma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka**}. Ninashuhudia kuwa, hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika. Na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu teremsha rehma na amani pamoja na baraka kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale waliowafuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

**Baada ya Utangulizi**:

Kuimarisha maadili mema ndani ya jamii ni dalili ya ustawi na maendeleo yake, lakini ni siri ya kushikamana kwake na utulivu wake, kama vile kuporomoka kwa jamii kunaanza kuporomoka kwa mfumo wa maadili ya kijamii, kwani jamii ambazo hazina maandili mema zinabeba sababu za kuporomoka kwake, kwa sababu jamii hizo zinasimama kwenye msingi wenye kutikisika kama anavyosema Mshairi: **إِنَّمَا الأُمَمُ الأَخْلاقُ ما بَقِيَتْ *** فإنْ همُ ذَهَبَتْ أَخْلاقُهُمْ ذَهَبُوا** *Watu wenye maadili mema bado wamebakia **** Pindi maadili yao mema yanapoondoka nao wao wanaondoka*.

Hakuna shaka kuwa dini yetu ya kati na kati imetoa uzito mkubwa kwenye maadili mema ya kijamii ambayo yanalinda umbile la jamii, na kuzipa nguvu nguzo zake,

hilo ni kwa sababu kulinda na kuhifadhi maadili mema na tabia njema ni msingi wa dini hii tukufu, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: **إنما بُعِثْتُ لأُتَمِّمَ مكارمَ الأخلاقِ** kwa maana: "*Nimeletwa ili kutimiliza maadili mema*".

Miongoni mwa maadili haya ya kijamii: Ni msingi wa kusaidiana na kuishi pamoja, maisha ambao yanarudisha manufaa kwa jamii yote, kwani nchi ni ya wananchi wote pasi ya kutafautisha kwa msingi wa dini au rangi au utaifa, na katika hilo ni pamoja na kupingi ubinafsi na kujipendelea, lakini pia kuimarisha msingi wa undugu wa kibinadamu jambo ambalo linazalisha ndani ya jamii mshikamano unaosimama juu upendo na kutoa, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى وَلا تَعَاوَنُوا عَلَى الإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ .**

{**Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui**} na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W:

**مثلُ المؤمنين في تَوادِّهم، وتَرَاحُمِهِم، وتعاطُفِهِمْ مثلُ الجسَدِ، إذا اشتكَى منْهُ عضوٌ تداعَى لَهُ سائِرُ الجسَدِ بالسَّهَرِ والْحُمَّى .**

"*Mfano wa Waumin katika kupenda kwao na kuoneana kwao huruma na kusaidiana kwao ni mfano wa mwili, pindi kiungo cha mwili kinapopata maumivu basi hupelekea mwili wote kukesha kwa maumivu na homa*". Na anasema Mtume S.A.W:

**إِنَّ الأَشْعَرِيِّينَ إِذَا أَرْمَلُوا فِي الغَزْوِ ، أَوْ قَلَّ طَعَامُ عِيَالِهِمْ بِالْمَدِينَةِ جَمَعُوا مَا كَانَ عِنْدَهُمْ فِي ثَوْبٍ وَاحِدٍ ، ثُمَّ اقْتَسَمُوهُ بَيْنَهُمْ فِي إِنَاءٍ وَاحِدٍ بِالسَّوِيَّةِ ، فَهُمْ مِنِّي وَأَنَا مِنْهُمْ.**

"*Watu wa kabila la Ash'ariy pindi wanapoishiwa vitu vyao wakiwa vitani au kupungukiwa na chakula cha familia zao, basi hukusanya walichonacho kwenye nguo moja kisha wanagawana kati yao kwenye chombo kwa usawa, basi wao ni katika mimi na mimi ni kati wao*".

Miongoni mwa maadili ya kijamii: Ni tabia ya uungwana murua na kujitoa, jambo linaloongeza mshikamano wa kitaifa na kijamii, na kuleta upendo na undugu pamoja na utulivu kati ya wanajamii, na hili ni katika aliyoliashiria Mtume S.A.W pale alipokataza kufanyiana maudhi husuda na kukatana, ambapo anasema Mtume S.A.W:

**لَا تَحَاسَدُوا ، وَلَا تَنَاجَشُوا ، وَلَا تَبَاغَضُوا ، وَلَا تَدَابَرُوا، وَلَا يَبِعْ بَعْضُكُمْ عَلَى بَيْعِ بَعْضٍ.**

"*Wala musifanyiane husuda wala musiongezeane bei kwenye minada wala musileteane chuki wala musiuziane baadhi yenu kwa kitu walishapatana bei*". Na anasema tena Mtume:

**وَمَنْ كَانَ فِي حَاجَةِ أَخِيهِ كَانَ اللَّهُ فِي حَاجَتِهِ، وَمَنْ فَرَّجَ عَنْ مُسْلِمٍ كُرْبَةً فَرَّجَ اللَّهُ عَنْهُ كُرْبَةً مِنْ كُرُبَاتِ يَوْمِ القِيَامَةِ، وَمَنْ سَتَرَ مُسْلِمًا سَتَرَهُ اللَّهُ يَوْمَ القِيَامَةِ.**

"*Mtu mwenye kushuhurishwa na kusaidia ngugu yake Mwenyezi Mungu anakuwa kwenye mahitaji yake, na mwenye kumuondolea Muislamu tatizo Mwenyezi Mungu atamuondolea matatizo siku ya kiyama, na mwenye kumsitiri Muislamu Mwenyezi Mungu naye atamsitiri siku ya kiyama*".

Miongoni mwa maadili pia: Ni uzito wa uangalizi kwa watu wenye matatizo mayatima wanyonge na wazee, kwa kuzingatia kuwa kuwaangalia vizuri ni jambo la lazima kidini kitaifa na kibinadamu, ambapo anasema Mtume wetu Muhammad SAW: **السَّاعِي علَى الأرْمَلَةِ والمِسْكِينِ كالْمُجاهِدِ في سَبيلِ اللَّهِ، أوْ كالَّذِي يَصُومُ النَّهارَ ويقومُ اللَّيْلَ**

"*Mwenye kumsaidia mjane na masikini ni kama mpiganji jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, au ni kama yule mwenye kufunga mchana na kusimama usiku kwa ajili ya ibada*" kama vile Uislamu umezingatia kuwafanikishia watu wenye matatizo ni nguvu ya ziada ya jamii, na kigezo kwa wengine na kutoa nafasi ya kusimama kwa nafasi zao katika maisha ya kijamii, kwa sababu hiyo Abdillah Ibn Umma Maktum R.A alikuwa muadhini wa Mtume wetu S.A.W kama vile alimtanguliza kwenye mji wa Madina mara nyingi ili kuwaswalisha watu na kuangalia hali zao.

*****

**Hotuba ya Pili:**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Miongoni mwa maadili muhimu ya kijamii: Ni tabia ya kuchunguza na kuthibitisha habari kabla ya kuieneza, kwani Sharia ya Kiislamu imesisitiza juu ya tabia hii njema, na ikatahadharisha na maneno ya uzushi na wasambazaji wake, kwa kuzingatia kuwa kueneza uzushi lengo lake ni kuharibu jamii, na kufanya kazi ya kueneza hali ya ukatishaji tama kati ya wana jamii, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنُوا أَنْ تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَى مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ.**

{**Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na habari yeyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda**}. Na anasema Mtume wetu S.A.W: **كَفَى بِالْمَرْءِ كَذِبًا أَنْ يُحَدِّثَ بِكُلِّ مَا سَمِعَ** "*Inatosha kwa mtu kupata dhambi kwa kuzungumza kila anachokisikia*". Mtu mwenye akili hufikiri kabla ya kuzungumza, na mtu mjinga huzungumza pasi ya kufikiri, na anasema tena Mtume Muhammad S.A.W:

**وَمَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَاليَوْمِ الآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ.**

"*Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi na azungumze mazuri au anyamaze*".

Ni uzuri ulioje kushikamana na maadili mema ya kijamii ili kufikia mshikamano kati ya wanajamii wote.

Ewe Mwenyezi Mungu tuongoze kwenye tabia zilizo nzuri zaidi, kwani hakuna wa kutuongoze kwenye tabia hizo ispokuwa ni Wewe tu.